# ULIZA NIKUJIBU

# SEHEMU YA KWANZA: <u>TUNASADIKI</u>

## TUNASADIKI KWA MUNGU MMOJA

***1 - Asili ya uhai wote ni nani?***
- Asili ya uhai wote ni Mwenyezi Mungu. "Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi" *(Mwa 1:1).*

***2 - Mungu aliumbaje vyote?***
- Mungu aliumba vyote kwa kutaka tu, bila ya kutumia chochote. "Nakusihi, mwanangu, inua macho yako utazame mbingu na nchi, ukaone vitu vyote vilivyomo; fahamu kwamba Mungu hakuviumba kwa vitu

vilivyokuwapo. Na ndivyo alivyofanya wanadamu pia" *(2Mak 7:28).* Umuambie: "Najua ya kuwa waweza kufanya mambo yote, na ya kuwa makusudi yako hayawezi kuzuilika" *(Ayu 42:2).*

***3 - Kwa nini Mungu aliumba vyote?***

- Mungu aliumba vyote bila ya kulazimika, kusudi tu adhihirishe na kushirikisha utukufu wake. "Mbingu zauhubiri utukufu wa Mungu, na anga laitangaza kazi ya mikono yake" *(Zab 19:1).* "Kwa kuwa vitu vyote vyatoka kwake, viko kwa uweza wake, tena vinarejea kwake. Utukufu una yeye milele. Amina" *(Rom 11:36).*

***4 - Je, Mungu anazidi kushughulikia viumbe vyake?***

- Ndiyo, Mungu anazidi kushughulikia viumbe vyake, akividumisha na kuviongoza vyote vifikie lengo alilovipangia. "Ndani yake yeye tunaishi, tunakwenda na kuwa na uhai wetu" *(Mdo. 17:28).* Tunamtegemea pande zote: angetuacha kidogo tungetoweka mara. Yesu alipolaumiwa kwa kuponya watu siku ya pumziko, alijitetea kwamba, "Baba yangu anatenda kazi hata sasa, nami ninatenda kazi" *(Yoh. 5:17).* "Yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu" *(1Pet. 5:7).*

***5 - Ikiwa Mungu anatushughulikia, tunapaswa kufanya nini?***

- Ikiwa Mungu anatushughulikia, tunapaswa kujiachilia mikononi mwake kwa moyo wa kitoto, tukiwajibika bila ya mahangaiko yanayowapata watu wasiomjua. "Waangalieni ndege wa angani, ya kwamba hawapandi, wala hawavuni, wala hawakusanyi ghalani; na Baba yenu wa mbinguni huwalisha hao. Ninyi je, si bora kupita hao?" *(Math 6:26).* "Nawe una nini usichokipokea?" *(1Kor 4:7).* "Nimrudishie Bwana nini kwa ukarimu wake wote alionitendea?" *(Zab 116:12).*

***6 - Kwa kuwa tumetoka kwa Mungu na tutarudi kwake, tunapaswa kuishi vipi?***

- Kwa kuwa tumetoka kwa Mungu na tutarudi kwake, tunapaswa kuishi

kulingana na hakika hiyo, kwa kumpa daima nafasi ya kwanza katika mawazo na mapendo yetu, tusijali kiumbe chochote kuliko yeye wala badala yake. "Bwana, Mungu wetu, Bwana ndiye mmoja. Nawe mpende Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote" *(Kumb 6:4-5).* Tusipoitikia upendo wake na kuambatana naye, basi, tumeshindikana kabisa.

***7 - Tunaanzaje kumjua Mungu?***

- Tunaanza kumjua Mungu kwa kuzingatia viumbe vyake, hasa dhamiri yetu. "Kwa sababu mambo yake yasiyoonekana tangu kuumbwa ulimwengu yanaonekana, na kufahamika kwa kazi zake; yaani, uweza wake wa milele na Uungu wake" *(Rom 1:20).*

***8 - Je, tunaweza kusema juu ya Mungu?***

- Ndiyo, tunaweza kusema juu ya Mungu kuanzia wema, ukweli na uzuri wa viumbe vyake na kumsifu kiasi chetu kwamba ndiye wema, ukweli na uzuri wenyewe. Lakini tukiri pia kuwa maneno yetu duni hayawezi kutosha kamwe kufafanua fumbo lake. "Kwa maana, nimesema maneno nisiyoyafahamu, mambo ya ajabu ya kunishinda mimi, nisiyoyajua" *(Ayu 42:3).* Tungemuelewa, asingekuwa Mungu.

***9 - Mwenyezi Mungu yukoje basi?***

- Mwenyezi Mungu ni ukamilifu mtupu usio na mipaka kwa milele yote. "Tazama, Mungu ni mkuu, nasi hatumjui; hesabu ya miaka yake haitafutiki" *(Ayu 36:26).* "Mungu ni Roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli" *(Yoh 4:24).*

***10 - Mungu akiwa Roho, viungo ambavyo pengine anapewa vina maana gani?***

- Mungu akiwa Roho, viungo ambavyo pengine anapewa vinamaanisha tu sifa fulani: k.mf. macho ujuzi wake, mikono uwezo wake, mabawa ulinzi wake, n.k. "Roho haina mwili na mifupa" *(Lk 24:39).*

***11 - Je, Mungu amewasiliana nasi?***

- Ndiyo, Mungu amewasiliana nasi, akijitambulisha na kujitoa kwetu, tuweze kuishi katika urafiki naye na hatimaye tushiriki heri yake. "Nikiziangalia mbingu zako, kazi ya vidole vyako, mwezi na nyota ulizoziratibisha; mtu ni kitu gani hata umkumbuke, na binadamu hata umwangalie? Umemfanya mdogo punde kuliko Mungu; umemvika taji ya utukufu na heshima" *(Zab 8:3-5).* "Siwaiti tena watumwa; kwa maana mtumwa hajui atendalo bwana wake; lakini ninyi nimewaita rafiki, kwa kuwa yote niliyoyasikia kwa Baba yangu nimewaarifu" *(Yoh 15:15).*

***12 - Hasa Mungu amejifunua kuwa nani?***

- Hasa Mungu amejifunua kuwa upendo wenyewe. "Bwana, Bwana, Mungu mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli" *(Kut 34:6).* "Mungu ni upendo, naye akaaye katika pendo, hukaa ndani ya Mungu, na Mungu hukaa ndani yake" *(1Yoh 4:16).* "Yeye asiyependa, hakumjua Mungu, kwa maana Mungu ni upendo" *(1Yoh 4:8).*

***13 - Je, Mungu amejitambulisha pia kwa jina?***

- Ndiyo, Mungu amejitambulisha pia kwa majina mbalimbali. Katika Agano la Kale jina muhimu kuliko yote liliandikwa "YHWH" yaani, "Mimi Ndimi". Tangu zamani Wayahudi hawalitamki, hivyo wakilifikia wanasoma kwa kutafsiri, "Bwana". Ndiyo sababu katika Agano Jipya halitumiki kamwe, isipokuwa Yesu alifunua Umungu wake kwa kujisemea, "Mimi Ndimi" na kwa kukubali kuitwa, "Bwana". Pamoja na hayo, alisali na kufundisha kusali kwa kumuelekea "ABA" yaani, "Baba". Ndilo jina ambalo linampendeza zaidi na kutuingiza katika fumbo lake kama wana ndani ya Mwana pekee ambaye "Mungu alimwadhimisha mno, akamkirimia Jina lile lipitalo kila jina; ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi; na kila

ulimi ukiri ya kuwa Yesu Kristo ni Bwana, kwa utukufu wa Mungu Baba" *(Fil 2:9-11).* "Msalipo, semeni, 'Baba, jina lako litakaswe'" *(Lk 11:2).* "Mlipokea roho ya kufanywa wana, ambayo kwa hiyo twalia, 'Aba!' yaani, 'Baba!'" *(Rom 8:15).*

***14 - Mungu ametufunulia nini tena?***

- Mungu ametufunulia pia ukweli juu yetu wenyewe akijibu kabisa maswali yanayotusumbua kuhusu maana na lengo la maisha yetu. Amefanya hivyo kwa maneno na matendo yanayoshikamana sana kwa kuwa maneno yanafafanua matendo, nayo matendo yanathibitisha maneno. "Mungu hutaka watu wote waokolewe, na kupata kujua yaliyo kweli" *(1Tim 2:4).* "Mungu si mtu, aseme uongo" *(Hes 23:19).* Yeye hadanganyiki wala hadanganyi.

***15 - Mungu akiwa wema mkuu na mwenye uwezo wote, mbona katika viumbe vyake kuna ubaya?***

- Mungu akiwa wema mkuu na mwenye uwezo wote, hakuumba ubaya wowote. Tena kila anapovumilia ule uliosababishwa na viumbe vyenye hiari anaufanya uzae mema makubwa zaidi kwa njia tusizoweza kuzifahamu vizuri hapa duniani. "Mimi ni Yusufu, ndugu yenu, ambaye mliniuza kwenda Misri. Basi sasa, msihuzunike, wala msiudhike nafsi zenu, kwa kuniuza huku; maana Mungu alinipeleka mbele yenu kuhifadhi maisha ya watu... Nanyi kweli mlinikusudia mabaya, bali Mungu aliyakusudia kuwa mema, ili itokee kuokoa taifa kubwa, kama ilivyo leo" *(Mwa 45:4-5; 50:20).*

***16 - Viumbe vyenye hiari ni vipi?***

- Malaika na watu ndio viumbe pekee vyenye hiari ya kuchagua wenyewe wachangie mpango wa Mungu au la. "Nazishuhudiza mbingu na nchi juu yenu hivi leo, kuwa nimekuwekea mbele yako uzima na mauti, baraka na laana; basi, chagua uzima, ili uwe hai, wewe na uzao wako; kumpenda Bwana, Mungu wako, kuitii sauti yake, na kushikamana naye; kwani hiyo ndiyo uzima wako" *(Kumb 30:19-20).*

***17 - Malaika na watu wanaweza kuchagua hata nini?***

- Malaika na watu wanaweza kuchagua hata wawe wema au wabaya milele. "Kulikuwa na vita mbinguni: Mikaeli na malaika zake wakapigana na yule joka, yule joka naye akapigana nao pamoja na malaika zake; nao hawakushinda, wala mahali pao hapakuonekana tena mbinguni" *(Ufu 12:7-8).* Chaguo letu binadamu linafanyika siku kwa siku kwa kuchukua misimamo mizuri au mipotovu kuhusu dini na maadili. "Mwayachunguza Maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayonishuhudia. Wala hamtaki kuja kwangu mpate kuwa na uzima" *(Yoh 5:39-40).*

***18 - Je, kati ya viumbe mbalimbali Mungu ameweka mpango wowote?***

- Ndiyo, kati ya viumbe mbalimbali Mungu ameweka mpango: alitaka malaika wasioonekana wamtumikie kwa kutusaidia sisi watu, na vile vinavyoonekana tuvitumie kwa uadilifu ili kwa njia yetu vimtukuze yeye. "Atakuagizia malaika zake wakulinde katika njia zako zote" *(Zab 91:11).* "Kwa Hekima yako ulimwumba mwanadamu, ili avitawale viumbe vilivyoumbwa nawe, na kumiliki ulimwengu katika utakatifu na kwa haki" *(Hek 9:2-3).*

***19 - Malaika wakoje?***

- Malaika ni roho tupu walioumbwa na Mungu ili wamtukuze milele, wamlinde kila mtu na kumtumikia Bwana Yesu katika kutuokoa. "Angalieni, msidharau mmojawapo wadogo hawa, kwa maana nawaambia ya kwamba malaika zao mbinguni sikuzote huutazama uso wa Baba yangu aliye mbinguni" *(Math 18:10).*

***20 - Sisi binadamu tukoje?***

- Sisi binadamu ni umoja wa mambo mawili: roho iliyoumbwa na Mungu moja kwa moja, na mwili ulioumbwa naye kwa njia ya wazazi. Maumbile

hayo yanatakiwa kukamilika kwa kupokea na kutimiza upendo wa Mungu aliyesema, "'Na tufanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi'. Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba" *(Mwa 1:26-27).*

***21 - Je, mwili wetu ni muhimu?***

- Ndiyo, mwili wetu ni muhimu, kwa sababu umeumbwa na Mungu, umetwaliwa na Mwanae ili atuokoe, umehuishwa na Roho Mtakatifu atakayeutukuza siku ya ufufuo kwa mfano wa Yesu. "Mwili si kwa zinaa, bali ni kwa Bwana, naye Bwana ni kwa mwili. Naye Mungu alimfufua Bwana, na tena atatufufua sisi kwa uweza wake. Je, hamjui ya kuwa miili yenu ni viungo vya Kristo? Basi nivitwae viungo vya Kristo na kuvifanya viungo vya kahaba? Hasha! Au hamjui ya kuwa yeye aliyeungwa na kahaba ni mwili mmoja naye?… Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu?" *(1Kor 6:13-16,19).*

***22 - Mungu aliwahi kujifunua kwa watu gani?***

- Mungu aliwahi kujifunua kwa wazazi wetu wa kwanza, akaendelea hasa kwa taifa la Israeli, hadi alipomtuma Mwanae ajifanye mtu wa taifa hilo teule. "Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana" *(Eb 1:1-2).*

***23 - Je, ufunuo wa Mungu unaendelea hata leo?***

- Hapana, ufunuo wa Mungu hauendelei, kwa sababu alikwisha kuukamilisha kwa kumtuma duniani Neno wake wa milele. "Kwa kuwa torati ilitolewa kwa mkono wa Musa; neema na kweli zilikuja kwa mkono wa Yesu Kristo. Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wowote; Mungu Mwana pekee aliye katika kifua cha Baba, huyu ndiye aliyemfunua" *(Yoh 1:17-18).* Baada yake hauwezekani ufunuo mpya. Hatutakiwi

kumuamini yeyote akidai eti, ametumwa kukamilisha kazi ya Yesu; kwa kuwa mwenyewe alisema, “Mbingu na nchi zitapita, lakini maneno yangu hayatapita kamwe” *(Math 24:35).* “Ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yoyote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na alaaniwe! Kama tulivyotangulia kusema, na sasa nasema tena, mtu awaye yote akiwahubiri ninyi injili yoyote isipokuwa hiyo mliyoipokea, na alaaniwe!” *(Gal 1:8-9).*

***24 - Ufunuo wa Mungu unatufikiaje miaka elfu mbili baada ya Kristo?***

- Ufunuo wa Mungu unatufikia kupitia Kanisa lake, lililokabidhiwa Mapokeo ya Mitume na linaloongozwa na Roho Mtakatifu hadi ukweli wote. Yesu aliahidi kwamba, “Yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake” *(Yoh 16:13).* “Maana Roho huchunguza yote hata mafumbo ya Mungu” *(1Kor 2:10).*

***25 - Mapokeo ya Mitume ndiyo nini?***

- Mapokeo ya Mitume ndiyo yale yote ambayo Yesu aliwakabidhi Mitume wake, na kwa uwezo wa Roho Mtakatifu yatadumu hata mwisho wa dunia katika mafundisho, liturujia na maisha ya Kanisa. “Nawasifu, kwa sababu mmenikumbuka katika mambo yote, nanyi mmeyashika yale mapokeo vilevile kama nilivyowatolea… Kwa maana naliwatolea ninyi hapo mwanzo yale niliyoyapokea mimi mwenyewe” *(1Kor 11:2; 15:3).* “Ilinde ile amana nzuri kwa Roho Mtakatifu akaaye ndani yetu… Mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine” *(2Tim 1:14; 2:2).* Tukikata huo mnyororo wa mapokeo, hata kama ni kwa kisingizio cha kushikilia Biblia, tunaachana na asili ya Kanisa. “Basi, ndugu, simameni imara, mkayashike mapokeo mliyofundishwa, ama kwa maneno, ama kwa waraka wetu… Ndugu, twawaagiza katika jina la Bwana Yesu Kristo, jitengeni nafsi zenu na kila ndugu aendaye bila

utaratibu, wala si kwa kufuata mapokeo mliyoyapokea kwetu" *(2Thes 2:15; 3:6).*

***26 - Maandiko Matakatifu ndiyo nini?***

- Maandiko Matakatifu ndiyo vitabu vyote 73 ambavyo viliandikwa na watu kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu vikakusanywa na Kanisa kwa jina la "Biblia", yaani "Vitabu". Hao "wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu" *(2Pet 1:21).*

***27 - Je, Biblia zote ni sawa?***

- Hapana, Biblia zote si sawa. Tujihadhari na matoleo mapungufu ambamo vimenyofolewa vitabu 7 vizima na sehemu kadhaa za vitabu vingine vilivyotumiwa na Wakristo wa kwanza. "Amin, nawaambia, mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka, hata yote yatimie" *(Math 5:18).* "Na mtu yeyote akiondoa lolote katika maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mungu atamwondolea sehemu yake katika ule mti wa uzima, na katika ule mji mtakatifu, ambao habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki" *(Ufu 22:19).*

***28 - Tunatambuaje Maandiko Matakatifu kati ya maandishi yote ya binadamu?***

- Tunatambua Maandiko Matakatifu kati ya maandishi yote ya binadamu kwa njia ya Mapokeo, yaani kwa sababu yametumiwa na Kanisa tangu mwanzo kwa kulisha kwa hakika imani yake. Tunahitaji Mapokeo kwa kuwa Maandiko yenyewe hayataji orodha ya vitabu vyake vyote, Sanasana Yesu alividokeza baadhi akisema yanamzungumzia na kutimia ndani yake, "Ni lazima yatimizwe yote niliyoandikiwa katika Torati ya Musa, na katika Manabii, na Zaburi" *(Lk 24:44).* Halafu Barua ya Pili ya Mtume Petro ikalinganisha "na Maandiko mengine" nyaraka zote ambazo Paulo aliziandika "kwa hekima aliyopewa" *(2Pet 3:15-16).*

***29 - Sababu nyingine za Biblia kutojitosheleza ni zipi?***

- Sababu nyingine za Biblia kutojitosheleza ni kwamba mambo mengi muhimu hayakuandikwa, "Kuna mambo mengine mengi aliyoyafanya Yesu, ambayo yakiandikwa moja moja, nadhani hata ulimwengu usingetosha kwa vile vitabu vitakavyoandikwa" *(Yoh 21:25).* Tena barua ni nusu tu ya kuonana; hivyo Yesu hakuandika lolote, nao Mitume hawakupenda kuandika yote. "Kwa kuwa ninayo mambo mengi, sitaki kuyaandika kwa karatasi na wino; lakini nataraji kuja kwenu, na kusema nanyi mdomo kwa mdomo, ili furaha yetu iwe imetimizwa" *(2Yoh 12).* "Nalikuwa na mambo mengi ya kukuandikia, lakini sipendi kukuandikia kwa wino na kalamu. Lakini nataraji kukuona karibu, nasi tutasema mdomo kwa mdomo" *(3Yoh 13-14).* Hasa ibada haziwezi kufanyika kwa barua; k.mf. kuwekea mikono ili kumshirikisha Roho Mtakatifu. Paji la namna hiyo halipitii Maandiko, bali Mapokeo tu. Hatimaye Biblia ikipotoshwa haipingi, kwa kuwa si mtu hai anayeweza kujitetea.

***30 - Biblia iliandikwa kwa kusudi gani?***

- Biblia iliandikwa kusudi tupate "kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini" tuwe "na uzima wa milele" *(Yoh 20:31).* "Tangu utoto umeyajua Maandiko Matakatifu, ambayo yaweza kukuhekimisha hata upate wokovu kwa imani iliyo katika Kristo Yesu. Kila Andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki" *(2Tim 3:15-16).* Si lengo lake kutufundisha historia, jiografia wala sayansi: kuhusu elimu hizo na kuhusu ufasaha wa lugha Biblia ilitegemea ujuzi na vipawa vya watu walioiandika.

***31 - Je, vitabu vya Biblia vinatofautiana?***

- Ndiyo, vitabu vya Biblia vinatofautiana kwa kuwa Mungu alijifunua hatua kwa hatua; hivyo vitabu 46 vilivyoandikwa kabla ya Yesu vinaitwa Agano la Kale na 27 vilivyomfuata vinaitwa Agano Jipya. "Kwa kule

kusema, Agano jipya, amelifanya lile la kwanza kuwa kuukuu. Lakini kitu kianzacho kuwa kikuukuu na kuchakaa ki karibu na kutoweka" *(Eb 8:13).* Mungu "ndiye aliyetutosheleza kuwa wahudumu wa agano jipya; si wa andiko, bali wa roho; kwa maana andiko huua, bali roho huhuisha" *(2Kor 3:6).*

***32 - Je, vitabu vyote vya Biblia vinahusiana?***

- Ndiyo, vitabu vyote vya Biblia vinahusiana kwa kuwa vinaangaziana na kuunda kitabu kimoja ambacho ni Neno la Mungu yuleyule, ingawa katika hatua tofauti: Agano la Kale ndiyo maandalizi na Agano Jipya ndio utimilifu wake. Yesu alisema, "Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua Torati au Manabii; la, sikuja kutangua, bali kutimiliza" *(Math 5:17).* Tunahitaji Agano la Kale ili tuelewe vizuri Agano Jipya katika maandalizi yake, na tunahitaji Agano Jipya ili tuelewe Agano la Kale lilivyotimilizwa na Yesu.

***33 - Je, inafaa tushike neno lolote la Agano la Kale kama Wayahudi?***

- Hapana, haifai tushike neno lolote la Agano la Kale kama Wayahudi wasiozingatia jinsi Yesu alivyolitimiliza kwa maneno na matendo hata wakamshutumu kutenda kinyume: "Mtu huyo hakutoka kwa Mungu, kwa sababu haishiki sabato" *(Yoh 9:16).* Alipofafanua amri 10 za Mungu alikariri: "Mmesikia watu wa kale walivyoambiwa… lakini mimi nawaambieni…" *(Math 5:21,27,31,33,38,43).* Alipouliziwa unajisi wa vyakula kadhaa, alisisitiza, "'Hivi hata ninyi hamna akili? Hamfahamu ya kwamba kila kitu kilicho nje ya mtu, kikimwingia, hakiwezi kumtia unajisi; kwa sababu hakimwingii moyoni, ila tumboni tu; kisha chatoka kwenda chooni?' Kwa kusema hivi alivitakasa vyakula vyote" *(Mk 7:18-19).* "Basi, mtu asiwahukumu ninyi katika vyakula au vinywaji, au kwa sababu ya sikukuu au mwandamo wa mwezi, au sabato; mambo hayo ni kivuli cha mambo yajayo; bali mwili ni wa Kristo" *(Kol 2:16-17).* Hakika, mwili ni mzito kuliko kivuli chake.

***34 - Yesu alitimiliza Agano la Kale kwa namna isiyotarajiwa hasa lini?***

- Yesu alitimiliza Agano la Kale kwa namna isiyotarajiwa hasa aliposulubiwa, akionekana na Wayahudi wenzake kama kwamba amelaaniwa: "Kristo alitukomboa katika laana ya torati, kwa kuwa alifanywa laana kwa ajili yetu; maana imeandikwa: 'Amelaaniwa kila mtu aangikwaye juu ya mti'; ili kwamba baraka ya Ibrahimu iwafikilie Mataifa katika Yesu Kristo, tupate kupokea ahadi ya Roho kwa njia ya imani" *(Gal 3:13-14).*

***35 - Kati ya vitabu vya Biblia, vilivyo bora ni vipi?***

- Kati ya vitabu vya Biblia, vilivyo bora ni Injili 4 zilizoandikwa na Mathayo, Marko, Luka na Yohane. Ndio moyo wa Maandiko Matakatifu yote, kwa kuwa ndizo shuhuda kuu juu ya maisha na mafundisho ya Yesu. Yeye "amepata huduma iliyo bora zaidi, kwa kadiri alivyo mjumbe wa agano lililo bora, lililoamriwa juu ya ahadi zilizo bora. Maana kama lile la kwanza lingalikuwa halina upungufu, nafasi isingalitafutwa kwa lile la pili" *(Eb 8:6-7).*

***36 - Tueleweje Maandiko Matakatifu?***

- Tuelewe Maandiko Matakatifu kwa kuzingatia hasa Mungu alitaka kusema nini kuhusu wokovu wetu kupitia waandishi wengi aliowaongoza kuyatunga kwa lugha na mitindo mbalimbali. Lakini ebu, "Yamo mambo ambayo ni vigumu kuelewa nayo; na mambo hayo watu wasio na elimu, wasio imara, huyapotoa, kama vile wayapotoavyo na Maandiko mengine, kwa uvunjifu wao wenyewe" *(2Pet 3:16).* Utitiri wa madhehebu yanayoshindana yakidai kushikilia Biblia tu unathibitisha uwekezano mkubwa wa kuipotosha kwa namna moja au nyingine. "Utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima; ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia walimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti; nao watajiepusha wasisikie yaliyo kweli, na kuzigeukia

hadithi za uongo" *(2Tim 4:3-4).* Njia pekee ya kukwepa fujo hiyo ni kuelewa Maandiko ndani ya Kanisa, kadiri ya Mapokeo yake hai. "Lakini mtu yeyote akitaka kuleta fitina, sisi hatuna desturi kama hiyo, wala makanisa ya Mungu" *(1Kor 11:16).* Biblia nje ya Kanisa ni kama samaki nje ya maji.

***37 - Je, ufunuo wa Mungu unaweza kufafanuliwa rasmi na kila mtu?***

- Hapana, ufunuo wa Mungu unaweza kufafanuliwa rasmi na umoja wa Maaskofu tu, kwa kuwa ndio waandamizi wa Mitume 12 wa Yesu. "Au je, neno la Mungu lilitoka kwenu? Au kuwafikia ninyi peke yenu?" *(1Kor 14:36).* "Hakuna unabii katika Maandiko upatao kufasiriwa kama apendavyo mtu fulani tu. Maana unabii haukuletwa popote kwa mapenzi ya mwanadamu" *(2Pet 1:20-21).* Tunahitaji unyenyekevu wa Mwafrika ambaye shemasi Filipo alimsikia "anasoma chuo cha nabii Isaya; akanena, 'Je, yamekuelea haya unayosoma?' Akasema, "Nitawezaje kuelewa, mtu asiponiongoza?' Akamsihi Filipo apande na kuketi pamoja naye" *(Mdo 8:30-31).*

***38 - Tupokeeje ufunuo wa Mungu?***

- Tupokee ufunuo wa Mungu kwa kusadiki mafundisho ya Kanisa lake, ili tuzidi kumjua na kuambatana naye bila ya kudanganyika. Yesu aliwaambia Mitume wake, "Awasikilizaye ninyi anisikiliza mimi, naye awakataaye ninyi anikataa mimi; naye anikataaye mimi amkataa yeye aliyenituma" *(Lk 10:16).* "Sisi nasi twamsukuru Mungu bila kukoma, kwa kuwa, mlipopata lile neno la ujumbe la Mungu mlilolisikia kwetu, mlilipokea si kama neno la wanadamu, bali kama neno la Mungu; na ndivyo lilivyo kwelikweli, litendalo kazi pia ndani yenu ninyi mnaoamini" *(1Thes 2:13).*

***39 - Tunaweza kusadiki vipi?***

- Tunaweza kusadiki kwa msaada wa Roho Mtakatifu tu,

anayetuelekeza kwa Mungu, akituangazia Neno lake na kutuvuta tulikubali kwa moyo. "Mtu akipenda kuyatenda mapenzi yake, atajua habari ya yale mafunzo, kwamba yatoka kwa Mungu" *(Yoh 7:17).* "Nanyi mmepakwa mafuta na Yeye aliye Mtakatifu kweli, nanyi mnajua nyote" *(1Yoh 2:20).* Kumbe, "Mwanadamu wa tabia ya asili hayapokei mambo ya Roho wa Mungu; maana kwake huyo ni upuzi, wala hawezi kuyafahamu, kwa kuwa yatambulikana kwa jinsi ya rohoni" *(1Kor 2:14).*

***40 - Je, miujiza inaweza kutusaidia tusadiki?***

- Ndiyo, miujiza inaweza kutusaidia tusadiki, lakini inaweza kutudanganya pia. "Wakati huo mtu akiwaambia, 'Tazama, Kristo yupo hapa', au, 'Yuko kule', msisadiki. Kwa maana watatokea makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu, wapate kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule" *(Math 24:23-24).* "Maana watu kama hao ni mitume wa uongo, watendao kazi kwa hila, wanaojigeuza wawe mfano wa mitume wa Kristo. Wala si ajabu. Maana Shetani mwenyewe hujigeuza awe mfano wa malaika wa nuru" *(2Kor 11:13-14).* Alipomshawishi Yesu alitumia hata maneno ya Biblia "akamwambia, 'Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu jitupe chini, kwa maana imeandikwa: Atakuagizia malaika zake, na mikononi mwao watakuchukua, usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe" *(Math 4:6).*

***41 - Kanisa linahusika vipi na imani?***

- Kanisa linahusika na imani kama mama wa waamini wote, kwa sababu imani yake inatangulia, inazaa, inategemeza na kulisha imani yetu: lenyewe ni "nguzo na msingi wa kweli" *(1Tim 3:15).* Tukiondoa nguzo na msingi, nyumba ya ukweli haiwezi kusimama. "Kila atakayeliitia Jina la Bwana ataokoka. Basi wamwiteje yeye wasiyemwamini? Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia? Tena wamsikieje pasipo mhubiri? Tena wahubirije, wasipopelekwa?… Basi imani, chanzo chake ni kusikia" *(Rom 10:13-15,17).* Hivyo wokovu unategemea kupokea kwa imani maneno ya watu hai waliotumwa rasmi, sio Biblia peke yake. Mitume

waliandika tu kwa kutegemeza mahubiri yao: "Sikuwaandikia ninyi kwa sababu hamwijui iliyo kweli, bali kwa sababu mwaijua, tena kwamba hapana uongo wowote utokao katika hiyo kweli" *(1Yoh 2:21).* "Nitakuwa tayari kuwakumbusha hayo sikuzote, ijapokuwa mnayajua na kuthibitishwa katika kweli mliyo nayo" *(2Pet 1:12).*

***42 - Je, tukipata mafundisho ya Kanisa tunapaswa kuyasadiki?***
- Ndiyo, tukipata mafundisho ya Kanisa tunapaswa kuyasadiki kwa moyo mmoja tupate uzima wa milele, kwa kuwa Yesu aliwaambia Mitume, "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa" *(Mk 16:16).*

***43 - Tunapaswa kusadiki hasa nini?***
- Tunapaswa kusadiki hasa Utatu wa Mungu pekee, kwamba ni Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Milele yote Baba kwa jinsi alivyo ndani mwake anamzaa Mwana na kumvuvia Roho Mtakatifu, kama vile jua linavyotoa mwanga na joto lisitenganike navyo. Mwana, ambaye "ni mng'ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake" *(Eb 1:3),* alisema: "Nimekuja kutupa moto duniani" *(Lk 12:49).* Naye Roho aliwashukia wafuasi wake "kama ndimi za moto uliowakalia kila mmoja wao. Wote wakajazwa Roho Mtakatifu" *(Mdo 2:3-4).*

***44 - Je, Mungu amegawanyika sehemu tatu?***
- Hapana, Mungu hagawanyiki hata kidogo, bali daima ni Umoja kamili. "Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja" *(Mk 12:29).* Tumuabudu yeye peke yake katika nafsi tatu, na Utatu wa nafsi katika Umoja wa hali yake, tusichanganye nafsi wala kugawa Umungu. Baba si Mwana wala Roho Mtakatifu. Mwana si Baba wala Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu si Baba wala Mwana. Lakini milele yote nafsi hizo tatu ni Mungu yuleyule pasipo tofauti ya kuzitenganisha: kila moja imo ndani ya nyingine. "Mimi na Baba tu umoja" *(Yoh 10:30).*

***45 - Tumejuaje kuwa Mungu ni Umoja wa nafsi tatu?***

- Tumejua kuwa Mungu ni Umoja wa nafsi tatu kwa sababu Baba aliwatuma kwetu Mwanae na Roho Mtakatifu. "Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama, mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake. Na tazama, sauti kutoka mbinguni ikisema, 'Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye'" *(Math 3:16-17).* Naye akaagiza, "Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu" *(Math 28:19).* Ni nafsi tatu zenye jina moja, yaani Umungu mmoja tu.

***46 - Umoja wa Mungu unategemea nini?***

- Umoja wa Mungu unategemea hasa kwamba Mwana na Roho Mtakatifu wanachanga Umungu wa Baba, ambaye wanatokana naye pasipo utengano wowote. Baba anajifahamu na kujipenda: wazo analojifahamu ndiye Mwana, upendo anaojipenda katika wazo hilo ndiye Roho Mtakatifu. "Baba, hao ulionipa nataka wawe pamoja nami popote nilipo, wapate na kuutazama utukufu wangu ulionipa; kwa maana ulinipenda kabla ya kuwekwa msingi ulimwengu" *(Yoh 17:24).*

***47 - Je, nafsi tatu za Mungu zina Umoja hata katika utendaji?***

- Ndiyo, nafsi tatu za Mungu zina Umoja hata katika utendaji, kila nafsi akiuchangia kulingana na sifa yake maalumu ndani ya Utatu. Baba Mwenyezi sifa yake ni Uwezo. Mwana kama Neno la Baba sifa yake ni Hekima. Roho kama Pumzi ya uhai ya Baba sifa yake ni Upendo. Katika Uwezo wake Baba anafanya yote kwa Hekima na Upendo, hasa katika utume wa Mwana aliyefanyika mtu na katika utume wa Roho kama paji. "Amin, amin, nawaambia: Mwana hawezi kutenda neno mwenyewe ila lile ambalo amwona Baba analitenda; kwa maana yote ayatendayo yeye, ndiyo ayatendayo Mwana vilevile" *(Yoh 5:19).*

***48 - Je, Mungu aliumba watu wa kwanza katika hali ya mateso na***

***mauti tuliyonayo sasa?***

- Hapana, Mungu aliumba watu wa kwanza katika hali ya heri, wakiwa na upendo wake, utakatifu na uadilifu. Mateso na mauti yametokana na uasi wetu ambao tangu mzazi wetu wa kwanza tunajaribu kuboresha maisha yetu mbali na Mungu. "Mungu hakuifanyiza mauti, wala haimpendezi walio hai wakipotea… Ila ulimwengu uliingiwa na mauti kwa husuda yake Shetani" *(Hek 1:13; 2:24).* "Dhambi iliingia ulimwenguni kwa mtu mmoja, na kwa dhambi hiyo mauti; na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi" *(Rom 5:12).*

***49 - Je, Mungu angeweza kuzuia watu wasitende dhambi?***

- Ndiyo, Mungu angeweza kuzuia watu wasitende dhambi, lakini aliwaacha watende kwa hiari yao awaonyeshe ukuu wa huruma yake. "Maana Mungu amewafunga wote pamoja katika kuasi ili awarehemu wote" *(Rom 11:32).*

***50 - Je, toka mwanzo sisi watu tunaasi mpango wa Mungu peke yetu?***

- Hapana, toka mwanzo sisi watu tunaasi mpango wa Mungu kwa kuvutwa na mashetani, yaani malaika waliokataa moja kwa moja kumtumikia; baada ya dhambi ya asili hao wanatutumia sisi pia tuangushane na wenzetu. Lakini Mungu aliwahi kumuambia Shetani: "Nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako, na uzao wake; huo utakuponda kichwa, na wewe utamponda kisigino" *(Mwa 3:15).* "Hata ulipowadia utimilifu wa wakati, Mungu alimtuma Mwanawe ambaye amezaliwa na mwanamke" *(Gal 4:4).*

***51 - Je, dhambi zote zinahusiana?***

- Ndiyo, dhambi zote zinahusiana kwa sababu dhambi zinazaa dhambi nyingine ndani mwetu na katika mazingira yetu. "Hamjui kwamba chachu kidogo hulichachusha donge zima? Basi, jisafisheni, mkatoe ile chachu ya kale, mpate kuwa donge jipya" *(1Kor 5:6-7).*

***52 - Dhambi zimetuathiri vipi tena?***

- Dhambi zimetuathiri kwa ndani zaidi, zikitutia udhaifu katika mwili, ujinga katika akili na uovu katika utashi; madonda hayo yanatufanya tuzidi kushindwa. "Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii" *(Rom 8:7).*

***53 – Katika unyonge wetu tutumainie nini?***

- Katika unyonge wetu tutumainie huruma ya Mungu aliyetutumia Mkombozi hata "dhambi ilipozidi, neema ikawa kubwa zaidi" *(Rom 5:20).* Ushindi wake juu ya dhambi umetupatia mema makubwa kuliko tuliyoyapoteza kwa dhambi. "Mungu, kwa kuwa ni mwingi wa rehema, kwa mapenzi yake makuu aliyotupenda; hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa ajili ya makosa yetu; alituuhisha pamoja na Kristo; yaani, mmeokolewa kwa neema" *(Ef 2:4-5).*

## TUNASADIKI KWA BWANA MMOJA, YESU KRISTO

***54 - Nani Mkombozi wa watu wote?***

- Mkombozi wa watu wote ni Yesu Kristo, Mwana pekee wa Mungu, Bwana wetu. "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele" *(Yoh 3:16).* "Katika yeye, tunao ukombozi, yaani, msamaha wa dhambi" *(Kol. 1:14).* "Yeye mwenyewe alizichukua dhambi

zetu katika mwili wake juu ya mti; ili, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi tuwe hai kwa mambo ya haki" *(1Pet 2:24).*

### *55 - Yesu maana yake nini?*

- Yesu maana yake ni "Mungu Mwokozi": alichaguliwa jina hilo kabla hajazaliwa, akitabiriwa kuwa "yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao" *(Math 1:21).* "Hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo" *(Mdo 4:12).*

### *56 - Kristo maana yake nini?*

- Kristo maana yake ni "Aliyepakwa mafuta" awe kiongozi wa taifa lake walivyotabiri manabii wa kale. Tunahitaji kujua "habari za Yesu wa Nazareti, jinsi Mungu alivyomtia mafuta kwa Roho Mtakatifu na nguvu" *(Mdo 10:38).*

### *57 - Yesu kuwa Mwana pekee wa Mungu maana yake nini?*

- Yesu kuwa Mwana pekee wa Mungu maana yake ni kwamba, kabla hajazaliwa kama mtu duniani ni Mungu, sawa na Baba anayemzaa yeye tu tangu milele. "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu… Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu… Amwaminiye yeye hahukumiwi, asiyemwamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu" *(Yoh 1:1,14; 3:18).*

### *58 - Je, anaweza mtu kusema, 'Yesu ni Bwana'?*

- Hapana, "hawezi mtu kusema, 'Yesu ni Bwana', isipokuwa katika Roho Mtakatifu" *(1Kor 12:3)* anayemtia imani ya kuwa huyo aliyetupwa na watu wake ametawazwa na Baba juu ya wote.

### *59 - Yesu ni Mungu au mtu?*

- Yesu ni Mungu na mtu kwa pamoja, ndiyo sababu ni mshenga pekee

kati ya Mungu na watu. "Kwa sababu Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, mwanadamu Kristo Yesu" *(1Tim 2:5).* "Katika yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili" *(Kol 2:9).* Hivyo ni Mungu kweli na mtu kweli.

***60 - Je, Umungu na utu wa Yesu vinachanganyikana?***

- Hapana, Umungu na utu wa Yesu vimeunganika katika nafsi moja visichanganyikane, kwa kuwa ndani yake hali hizo mbili zinatenda kila moja ya kwake. "Basi yule akida, aliyesimama hapo akimwelekea, alipoona ya kuwa alikata roho jinsi hii, akasema, 'Hakika mtu huyu alikuwa Mwana wa Mungu'" *(Mk 15:39).*

***61 - Je, Mwana wa Mungu tangu atwae mwili ni mtu kamili mwenye akili na utashi wa kibinadamu?***

- Ndiyo, Mwana wa Mungu tangu atwae mwili ni mtu kamili mwenye akili na utashi wa kibinadamu. Katika umoja wa nafsi yake vipawa hivyo vinatenda kulingana na Umungu anaouchanga na Baba na Roho Mtakatifu milele. "Hayo maneno niwaambiayo mimi siyasemi kwa shauri langu; lakini Baba akaaye ndani yangu huzifanya kazi zake" *(Yoh 14:10).*

***62 - Hapa duniani Yesu alizaliwa na nani?***

- Hapa duniani Yesu alizaliwa na Bikira Maria kama malaika alivyomuambia: "Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, na nguvu zake Aliye juu zitakufunika kama kivuli; kwa sababu hiyo, hicho kitakachozaliwa kitaitwa kitakatifu, Mwana wa Mungu" *(Lk 1:35).*

***63 - Malaika alimsalimia Maria "umejaa neema": maana yake nini?***

- Malaika alimsalimia Maria "umejaa neema" *(Lk 1:28)* maana ndiye tunda bora la ukombozi ulioletwa na Yesu. Kwa stahili za Mwanae alikingiwa asirithi kwa wazazi dhambi ya asili na madonda yanayotokana nayo, wala asitende dhambi maisha yake yote.

***64 - Kwa nini Maria anastahili kuitwa "Mama wa Mungu"?***

- Maria anastahili kuitwa "Mama wa Mungu" kwa sababu Mwana wa milele wa Mungu, ambaye ni Mungu sawa na Baba, alifanyika mtu toka kwake. Akiwa mja mzito alishangiliwa: "Umebarikiwa wewe katika wanawake, naye mzao wa tumbo lako amebarikiwa. Limenitokeaje neno hili, hata mama wa Bwana wangu anijilie mimi?" *(Lk 1:42-43).*

***65 - Kwa nini Mama wa Yesu anaitwa "Bikira daima"?***

- Mama wa Yesu anaitwa "Bikira daima" kwa sababu alimchukua mimba akiwa bikira, akamzaa bila ya kupotewa na ubikira, akabaki bikira hadi mwisho wa maisha yake. Hamu yake ya kuwa bikira hata kisha kuchumbiwa inajitokeza katika jibu alilompa malaika aliyemtabiria mimba: "Litakuwaje neno hili, maana sijui mume?" *(Lk 1:35).* Ni kielelezo cha Wakristo ambao Mtume Paulo aliwaandikia: "Nawaonea wivu, wivu wa Mungu; kwa kuwa naliwaposea mume mmoja, ili nimletee Kristo bikira safi" *(2Kor 11:2),* "mpate kumhudumia Bwana pasipo kuvutwa na mambo mengine" *(1Kor 7:35).*

***66 - Je, Maria amechangia wokovu wetu?***

- Ndiyo, Maria amechangia wokovu wetu kwa kukubali mpango wote wa Mungu aliyetaka amzae Mwanae, amlee na kumfuata kiaminifu hadi msalabani, aliposhiriki kumtoa kama sadaka ya kutuokoa. Msimamo wake ulikuwa mmoja tu: "Tazama, mimi ni mjakazi wa Bwana; na iwe kwangu kama ulivyosema" *(Lk 1:38).*

***67 - Je, Maria ni mama yetu pia?***

- Ndiyo, Maria ni mama yetu pia: kwa kushiriki kazi yote ya Mwanae, Adamu mpya, amekuwa Eva mpya, mama wa wale wote aliowakomboa msalabani. "Yesu alipomwona mama yake, na yule mwanafunzi aliyempenda amesimama karibu, alimwambia mama yake, 'Mama, tazama mwanao'. Kisha akamwambia yule mwanafunzi, 'Tazama, mama yako'" *(Yoh 19:26-27).* Kisha kushirikishwa ufufuko wake, anazidi kutushughulikia kimama tufike salama mbinguni alikotangulia kupalizwa

mwili na roho.

***68 - Je, ni vizuri kumsifu Maria?***

- Ndiyo, ni vizuri kumsifu Maria kwa imani yake kama alivyosifiwa na alivyotabiri mwenyewe: "'Heri aliyesadiki; kwa maana yatatimizwa aliyoambiwa na Bwana'… 'Tazama, tokea sasa vizazi vyote wataniita mbarikiwa'" *(Lk 1:45,48).* Ni lazima tulitimize hilo neno la Mungu katika kizazi chetu kama kilivyotimizwa na vizazi vilivyotangulia.

***69 - Je, ni muhimu kujua maisha ya Yesu?***

- Ndiyo, ni muhimu kujua maisha ya Yesu kwa sababu matendo na maneno yake, pamoja na kimya na sala yake, na hasa kifo na ufufuko wake, yote yanatufunulia Baba na matakwa yake kwetu. "Mambo ya Yesu wa Nazareti, aliyekuwa mtu nabii, mwenye uwezo katika kutenda na kunena mbele za Mungu na watu wote" *(Lk 24:19).*

***70 - Baada ya kujua maisha ya Yesu tunapaswa kufanya nini?***

- Baada ya kujua maisha ya Yesu tunapaswa kujilinganisha naye hadi aundwe na kuishi ndani mwetu akitushirikisha uhai, kifo na ufufuko wake. "Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu, na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu… Vitoto vyangu, ambao kwamba nawaonea utungu tena mpaka Kristo aumbike ndani yenu!" *(Gal 2:20; 4:19).*

***71 - Yesu alitumiaje sehemu kubwa ya maisha yake?***

- Yesu alitumia sehemu kubwa ya maisha yake kijijini akiwatii wazee wake Maria na Yosefu na kufanya kazi za mikono. "Alishuka pamoja nao mpaka Nazareti, naye alikuwa akiwatii" *(Lk 2:51).* Hivyo ametuachia kielelezo cha utakatifu katika maisha ya familia na ya kazi ambayo ndiyo njia ya kawaida ya kukomaa kiutu na kumtumikia Mungu. "Mnyenyekeane katika kicho cha Kristo" *(Ef 5:21).*

***72 - Lini Yesu aliacha maisha ya kijijini akaanza utume wake?***

- Yesu aliacha maisha ya kijijini akaanza utume wake miezi tu baada ya Yohane Mbatizaji, jamaa yake, kuwatikisa Wayahudi wote akihubiri wawe tayari kwa ujio wa mtu mkubwa zaidi, akisema, "Kweli mimi nawabatiza kwa maji kwa ajili ya toba; bali yeye ajaye nyuma yangu ana nguvu kuliko mimi, wala sistahili hata kuvichukua viatu vyake; yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa moto" *(Math 3:11).*

***73 - Kwa nini Yesu alishawishiwa na Shetani?***

- Yesu alishawishiwa na Shetani kwa kuwa ni mtu kweli, akamshinda kwa niaba ya watu wote, akituonyesha namna ya kumtii Mungu moja kwa moja, "hata mauti, naam, mauti ya msalaba" *(Fil 2:8).* "Kwa sababu kama kwa kuasi kwake mtu mmoja watu wengi waliingizwa katika hali ya wenye dhambi, kadhalika kwa kutii kwake mmoja watu wengi wameingizwa katika hali ya wenye haki" *(Rom 5:19).*

***74 - Kwa nini Yesu aliteswa hadi kuuawa msalabani?***

- Yesu aliteswa hadi kuuawa msalabani ili abebe kwa upendo na kufidia dhambi za watu wote, alivyotabiriwa: "Tulimdhania ya kuwa amepigwa, amepigwa na Mungu, na kuteswa. Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona" *(Isa 53:4-5).* Tangu mwanzo Wakristo wanakiri kwa ufupi kwamba, "Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo Maandiko" *(1Kor 15:3).* "Alijitoa nafsi yake kwa ajili yetu, ili atukomboe na maasi yote, na kujisafishia watu wawe milki yake mwenyewe, wale walio na juhudi katika matendo mema" *(Tit 2:14).* "Alijitoa mwenyewe kuwa ukombozi kwa ajili ya wote" *(1Tim 2:6).* "Ili kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani Ibilisi, awaache huru wale ambao kwamba maisha yao yote kwa hofu ya mauti walikuwa katika hali ya utumwa" *(Eb 2:14-15).*

***75 – Je, Mungu Baba alihusika na sadaka ya Mwanae?***

- Ndiyo, Mungu Baba alihusika sana na sadaka ya Mwanae, kwa sababu "Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake… Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika yeye" *(2Kor 5:19,21).*

***76 - Ajabu la ukombozi wa namna hiyo ni nini?***

- Ajabu la ukombozi wa namna hiyo ni kwamba, "tulipokuwa adui tulipatanishwa na Mungu kwa mauti ya Mwana wake" *(Rom 5:10).* "Hili ndilo pendo: si kwamba sisi tulimpenda Mungu, bali kwamba yeye alitupenda sisi, akamtuma Mwanae kuwa kipatanisho kwa dhambi zetu" *(1Yoh 4:10).* "Wala si kwa dhambi zetu tu, bali na kwa dhambi za ulimwengu wote" *(1Yoh 2:2).*

***77 - Kwa kuwa tumekombolewa kwa damu azizi ya Mwana wa Mungu, tunaonywa vipi?***

- Kwa kuwa tumekombolewa kwa damu azizi ya Mwana wa Mungu, tunaonywa kwamba, "Mlinunuliwa kwa thamani, sasa basi mtukuzeni Mungu katika miili yenu" *(1Kor 6:20).* "Kristo naye aliteswa kwa ajili yenu, akawaachia kielelezo, mfuate nyayo zake" *(1Pet 2:21)* katika kuvumilia na kusamehe. Ndivyo alivyofanya shemasi Stefano kwa waliompiga mawe mpaka akafa: "Akapiga magoti, akalia kwa sauti kuu, 'Bwana, usiwahesabie dhambi hii'. Akiisha kusema haya akalala" *(Mdo 7:60).*

***78 - Yesu alipokufa, ilikuwaje?***

- Yesu alipokufa, nafsi yake ya Kimungu iliendelea kushikamana na roho na mwili vilivyotengana: kwa hiyo mwili wake uliozikwa haukuweza kuoza kaburini; roho yake ilishukia kuzimu kuwatoa waadilifu waliomtangulia awaingize pamoja naye mbinguni. "Mwili wake aliuawa, bali roho yake akahuishwa, ambayo kwa hiyo aliwaendea roho waliokaa kifungoni, akawahubiri" *(1Pet 3:19).* "Roho yake haikuachwa kuzimu,

wala mwili wake haukuona uharibifu" *(Mdo 2:31).*

***79 - Siku ya tatu ilitokea nini?***

- Siku ya tatu roho ya Yesu ilirudi mwilini mwake na kudhihirisha utukufu wa ufufuko. Tangu mwanzo Wakristo wanakiri kwa ufupi "ya kuwa alizikwa; na ya kuwa alifufuka siku ya tatu, kama yanenavyo Maandiko" *(1Kor 15:4).*

***80 - Ufufuko wa Yesu siku ya Jumapili ulishuhudiwa na nani?***

- Ufufuko wa Yesu siku ya Jumapili ulishuhudiwa na malaika waliowaambia wanawake waliofika kaburini: "Kwa nini mnamtafuta aliye hai katika wafu? Hayupo hapa, amefufuka" *(Lk 24:5-6).* Halafu Maria Magdalena, Petro na Mitume wenzake, hata watu zaidi ya mia tano walimuona na kumsikia, walimgusa na kula pamoja naye.

***81 – Je, Yesu alirudia maisha ya duniani?***

- Hapana, Yesu hakurudia maisha ya duniani: tofauti na watu aliowafufua warudie maisha haya, Yesu mfufuka ameshaingia utukufu wa milele: "amekwenda zake mbinguni" *(1Pet 3:22),* "hafi tena" *(Rom 6:9),* ana "funguo za mauti, na za kuzimu" *(Ufu 1:18).*

***82 - Je, ufufuko wa Yesu ni muhimu kwetu pia?***

- Ndiyo, ufufuko wa Yesu ni muhimu kwetu pia, kwa sababu kwa njia yake tu tunatiwa uzima: sasa rohoni kwa kuondolewa dhambi, na siku ya mwisho mwilini pia kwa kufufuliwa. Mwenyewe alisema, "Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima. Yeye aniaminiye mimi ajapokufa, atakuwa anaishi; naye kila aishiye na kuniamini hatakufa kabisa hata milele" *(Yoh 11:25-26).* "Kristo amefufuka katika wafu, limbuko lao waliolala. Maana kwa kuwa mauti ililetwa na mtu, kadhalika na kiyama ya wafu ililetwa na mtu" *(1Kor 15:20-21).* "Alitolewa kwa ajili ya makosa yetu, na kufufuka ili tupate kuhesabiwa haki" *(Rom 4:25).*

***83 - Siku arubaini baada ya kufufuka, Yesu alifanya nini?***

- Siku arubaini baada ya kufufuka, Yesu alipaa mbinguni mbele ya wanafunzi wake. Hataonekana tena rasmi mpaka arudi siku ya mwisho. "Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni" *(Mdo 1:11).* "Mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu, Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu" *(Kol 3:1).*

***84 - Je, sisi tunahusika na kupaa kwake?***

- Ndiyo, sisi tunahusika na kupaa kwake, kwa sababu yeye ni kichwa chetu nasi ni viungo vya mwili wake: hivyo ametutangulia kwa Baba atuombee Roho Mtakatifu tukafike kwake. Mwenyewe ameahidi, "Mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi mwepo" *(Yoh 14:3).* "Ni nani atakayewashitaki wateule wa Mungu? Mungu ndiye mwenye kuwahesabia haki. Ni nani atakayewahukumia adhabu? Kristo Yesu ndiye aliyekufa; naam, na zaidi ya hayo, amefufuka katika wafu, naye yuko mkono wa kuume wa Mungu; tena ndiye anayetuombea" *(Rom 8:33-34).* "Yeye, kwa kuwa akaa milele, anao ukuhani wake usioondoka. Naye, kwa sababu hii, aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa yeye; maana yu hai sikuzote ili awaombee" *(Eb 7:24-25).*

***85 - Je, utawala wa Yesu umeshaanza?***

- Ndiyo, utawala wa Yesu umeshaanza nao utakamilika atakaporudi kuwahukumu wazima na wafu kwa kutenganisha moja kwa moja wema na wabaya. "Maana sharti amiliki yeye, hata awaweke maadui wake wote chini ya miguu yake. Adui wa mwisho atakayebatilishwa ni mauti" *(1Kor 15:25-26).* Hapo katikati "watafanya vita na Mwanakondoo, na

Mwanakondoo atawashinda, kwa maana Yeye ni Bwana wa Mabwana, na Mfalme wa Wafalme" *(Ufu 17:14).*

***86 - Utawala wa Yesu umeanza hasa wapi?***

- Utawala wa Yesu umeanza hasa katika Kanisa lake linalokusanya wale waliomuamini kuwa ni Bwana wakaokolewa. Mungu "alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake" *(Kol 1:13).* Yesu alisema, "Ufalme wangu sio wa ulimwengu huu… Mimi nimezaliwa kwa ajili ya haya, na kwa ajili ya haya mimi nalikuja ulimwenguni, ili niishuhudie kweli. Kila aliye wa hiyo kweli hunisikia sauti yangu" *(Yoh 18:36,37).* "Ufalme wa Mungu hauji kwa kuuchunguza" *(Lk 17:20).* "Ufalme wa mbinguni umefanana na chachu aliyoitwaa mwanamke, akaisitiri ndani ya pishi tatu za unga, hata ukachachwa wote pia" *(Math 13:33).* Baada ya kufufuka, aliwajibu Mitume waliomuuliza kuhusu wakati wa kurudisha ufalme: "Si kazi yenu kujua nyakati wala majira, Baba aliyoyaweka katika mamlaka yake mwenyewe. Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi" *(Mdo 1:7-8).*

# TUNASADIKI KWA ROHO MTAKATIFU

***87 – Roho Mtakatifu ni nani?***

- Roho Mtakatifu ni upendo wa Mungu, nafsi ya tatu ya Utatu Mtakatifu, mwenye Umungu mmoja na Baba na Mwana. "Pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi" *(Rom 5:5).* Ametumwa kwetu atufanyie kazi pasipo kuonekana. "Upepo huvuma upendako, na sauti yake waisikia, lakini hujui unakotoka wala unakokwenda; kadhalika na hali yake kila mtu aliyezaliwa kwa Roho" *(Yoh 3:8).* "Wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu" *(Rom 8:14).*

***88 – Je, kazi zote za Roho Mtakatifu zinahusiana na Yesu?***

- Ndiyo, kazi zote za Roho Mtakatifu zinahusiana na Yesu na kulenga hasa kuandaa watu wampokee, wamfuate na kumshuhudia katika umoja wa kundi lake, Kanisa. "Ajapo huyo Msaidizi, nitakayewapelekea kutoka kwa Baba, huyo Roho wa kweli atokaye kwa Baba, yeye atanishuhudia. Nanyi pia mnashuhudia" *(Yoh 15:26-27).*

***89 - Kanisa maana yake nini?***

- Kanisa maana yake ni "kusanyiko": ndani yake Roho Mtakatifu anaunganisha na Yesu na kati yao wale waliopokea Neno la Mungu na sakramenti zake. "Bwana alilizidisha Kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa… Na jamii ya watu walioamini walikuwa na moyo mmoja na roho moja" *(Mdo 2:47; 4:32).* Ndio tokeo la ombi la Yesu: "Wote wawe na umoja; kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako, hao nao wawe ndani yetu, ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma" *(Yoh 17:21).* Kumbe utitiri wa madhehebu yaliyotenganika unaleta picha ya "tawanyiko" ambayo inakwaza ulimwengu usisadiki. "Kila mtu wa kwenu husema, 'Mimi ni wa Paulo', na, 'Mimi ni wa Apolo', na, 'Mimi ni wa Kefa', na, 'Mimi ni wa

Kristo'. Je, Kristo amegawanyika?" *(1Kor 1:12-13).*

***90 - Je, Kanisa ni kundi la binadamu tu?***

- Hapana, Kanisa si kundi la binadamu tu, tunaloweza kulianzisha kama vile chama, timu n.k. Kanisa ni fumbo la Mwili wa Kristo unaohuishwa na Roho Mtakatifu. Kama Yesu linaonekana upande wa ubinadamu tu, kumbe linaunganisha utu na Umungu. Baba "alivitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya Kanisa, ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote" *(Ef 1:22-23).*

***91 - Je, tunaweza kuambatana na Yesu kwa kulikataa Kanisa?***

- Hapana, hatuwezi kuambatana na Yesu kwa kulikataa Kanisa, kwa kuwa hao wawili ni mwili mmoja, kama Bwanaarusi na Bibiarusi. "Hamkusoma ya kwamba yeye aliyewaumba mwanzo, aliwaumba mtu mume na mtu mke, akasema, 'Kwa sababu hiyo, mtu atamwacha babaye na mamaye, ataambatana na mkewe, na hao wawili watakuwa mwili mmoja'? Hata wamekuwa si wawili tena, bali mwili mmoja. Basi aliowaunganisha Mungu, mwanadamu asiwatenganishe" *(Math 19:4-6).* "Siri hiyo ni kubwa; ila mimi nanena habari ya Kristo na Kanisa" *(Ef 5:32).*

***92 - Je, Kanisa ni muhimu kwa wote?***

- Ndiyo, Kanisa ni muhimu kwa wote kwa kuwa ndilo ishara na chombo cha umoja wa watu na Mungu na kati yao. "Aliwapatanisha wote wawili na Mungu katika mwili mmoja, kwa njia ya msalaba, akiisha kuufisha ule uadui kwa huo msalaba. Akaja akahubiri amani kwenu ninyi mliokuwa mbali, na amani kwao wale waliokuwa karibu. Kwa maana kwa yeye sisi sote tumepata njia ya kumkaribia Baba katika Roho mmoja" *(Ef 2:16-18).*

***93 - Wokovu unapatikana wapi?***

- Wokovu unapatikana kwa Yesu tu, anayeishi katika Kanisa lake. Hata

hivyo Roho Mtakatifu anaweza akaongoza mtu asiyewajua bila ya kosa lake aungane nao kiroho kwa kumlenga Mungu na kujitahidi kumtii kwa moyo wote. "Tunamtumaini Mungu aliye hai, aliye Mwokozi wa watu wote, hasa wa waaminio" *(1Tim 4:10).* "Hakika natambua ya kuwa Mungu hana upendeleo; bali katika kila taifa mtu amchaye na kutenda haki hukubaliwa na yeye... Twaamini kwamba tutaokoka kwa neema ya Bwana Yesu vilevile kama wao" *(Mdo 10:34-35; 15:11).*

***94 - Mtu akijua Kanisa ni la lazima kwa wokovu asiingie au ajitenge nalo, itakuwaje?***

- Mtu akijua Kanisa ni la lazima kwa wokovu asiingie au ajitenge nalo hawezi kuingia mbinguni. "Roho anena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani; kwa unafiki wa watu wasemao uongo, wakichomwa moto dhamiri zao wenyewe" *(1Tim 4:1-2).* "Watoto, ni wakati wa mwisho. Na kama vile mlivyosikia kwamba mpinga Kristo yuaja, hata sasa wapinga Kristo wengi wamekwisha kuwapo. Kwa sababu hiyo twajua ya kuwa ni wakati wa mwisho. Walitoka kwetu, lakini hawakuwa wa kwetu. Maana kama wangalikuwa wa kwetu, wangalikaa pamoja nasi. Lakini walitoka ili wafunuliwe kwamba si wote walio wa kwetu" *(1Yoh 2:18-19).*

***95 - Je, anayejiunga na Kanisa na kudumu ndani yake ana hakika ya kuingia mbinguni?***

- Hapana, anayejiunga na Kanisa na kudumu ndani yake lakini haongozwi na Roho Mtakatifu kuishi kadiri ya ubatizo wake atahukumiwa na Mungu vikali zaidi kwa kuchezea neema kubwa hivi. "Kila aliyepewa vingi, kwake huyo vitatakwa vingi; naye waliyemwekea amana vitu vingi, kwake huyo watataka na zaidi" *(Lk 12:48).*

***96 - Sifa kuu za Kanisa ni zipi na zinapatikana wapi?***

- Sifa kuu za Kanisa ni kuwa moja, takatifu, katoliki na la Mitume. Sifa

hizo zinalitambulisha kati ya madhehebu mengi Kanisa pekee lililoanzishwa na Yesu kumpitia Mtume aliyembadilishia jina aitwe Petro, yaani Mwamba wa Kanisa lake lisilokoma wala kupotoka kamwe: "Wewe u Simoni, mwana wa Yohane; nawe utaitwa Kefa (tafsiri yake Petro)" *(Yoh 1:42).* Siku ya Pentekoste, "waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu" *(Mdo 2:41).* Ndiye aliyekaribisha hata wasio Wayahudi: "Tangu siku za kwanza Mungu alichagua miongoni mwenu ya kwamba Mataifa walisikie neno la Injili kwa kinywa changu, na kuliamini" *(Mdo 15:7).* Baada ya kuongoza Mitume wenzake na Kanisa lote, aliuawa msalabani huko Roma kama alivyotabiriwa: "'Utakapokuwa mzee, utainyosha mikono yako, na mwingine atakufunga na kukuchukua usikotaka'. Akasema neno hilo kwa kuonyesha ni kwa mauti gani atakayomtukuza Mungu" *(Yoh 21:18-19).*

### *97 - Kanisa kuwa moja maana yake nini?*

- Kanisa kuwa moja maana yake ni "mwili mmoja na Roho mmoja": lina "Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja" *(Ef 4:4-5).* Yesu alisema, "Na kondoo wengine ninao. Ambao si wa zizi hili; na hao nao imenipasa kuwaleta; na sauti yangu wataisikia; kisha kutakuwako kundi moja na mchungaji mmoja" *(Yoh 10:16).* Hakuna Kanisa lingine, isipokuwa matawi ambayo yamekatika kwa kiasi tofauti, na yana uhai kadiri yanavyounganika bado na shina. Hata leo Kanisa Katoliki peke yake lina waamini wengi kuliko jumla ya madhehebu mengine ya Kikristo.

### *98 - Kanisa kuwa takatifu maana yake nini?*

- Kanisa kuwa takatifu maana yake ni kazi ya Mungu mtakatifu inayong'aa katika watakatifu wa mbinguni, hasa Bikira Maria. "Ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu; ninyi mliokuwa kwanza si taifa, bali sasa ni taifa la Mungu" *(1Pet 2:9-10).* "Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili

yake; ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika Neno; apate kujiletea Kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lolote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa" *(Ef 5:25-27).* Hata hivyo hapa duniani linaundwa na wakosefu pia: "Ufalme wa mbinguni umefanana na juya, lililotupwa baharini, likakusanya wa kila namna. Hata lilipojaa, walilivuta pwani, wakaketi, wakakusanya walio wema vyomboni, bali walio wabaya wakawatupa" *(Math 13:47-48).*

***99 - Kanisa kuwa katoliki maana yake nini?***

- Kanisa kuwa katoliki maana yake linaweza kuwatolea watu wote wa mahali pote na wa nyakati zote kweli zote za imani na vifaa vyote vya kufikia wokovu wa milele. "Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi. Na tazama, mimi nipo pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari" *(Math 28:18-20).*

***100 - Kanisa kuwa la Mitume maana yake nini?***

- Kanisa kuwa la Mitume maana yake limejengwa juu ya Mitume 12 wa Yesu na kuongozwa na waandamizi wao. "Ukuta wa mji ulikuwa na misingi kumi na miwili, na katika ile misingi majina kumi na mawili ya wale mitume kumi na wawili wa Mwanakondoo" *(Ufu 21:14).* "Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye Yesu Kristo mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni. Katika yeye jengo lote linaungamanishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana. Katika yeye ninyi nanyi mnajengwa pamoja kuwa maskani ya Mungu katika Roho" *(Ef 2:20-22).*

***101 - Kanisa limepewa na Yesu muundo gani?***

- Kanisa limepewa na Yesu wahudumu wenye daraja takatifu wanaoitwa makleri; waamini wengine wanaitwa walei. Kutoka pande hizo mbili

wanapatikana watawa waliowekwa wakfu kwa namna ya pekee kwa kushika mashauri ya Kiinjili. Yesu "alipanda mlimani, akawaita aliowataka mwenyewe; wakamwendea. Akaweka watu kumi na wawili, wapate kuwa pamoja naye, na kwamba awatume kuhubiri" *(Mk 3:13-14).* "Walipoingia, wakapanda orofani, walipokuwa wakikaa; Petro, na Yohane, na Yakobo, na Andrea, Filipo na Tomaso, Bartholomayo na Mathayo, Yakobo wa Alfayo, na Simoni Zelote, na Yuda wa Yakobo. Hawa wote walikuwa wakidumu kwa moyo mmoja katika kusali, pamoja nao wanawake, na Mariamu mama yake Yesu, na ndugu zake" *(Mdo 1:13-14).*

***102 - Je, Yesu amejenga Kanisa lake imara juu ya mwamba?***

- Ndiyo, Yesu amejenga Kanisa lake imara juu ya Mtume Petro, alichunge lote kwa niaba yake. Papa kama Askofu wa Roma ndiye mwandamizi wa Petro na mkuu wa kundi zima la Maaskofu, waandamizi wa Mitume. "Wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu, wala milango ya kuzimu haitalishinda" *(Math 16:18).* "Atafananishwa na mtu mwenye akili, aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba. Mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile, isianguke; kwa maana misingi yake imewekwa juu ya mwamba" *(Math 7:24-25).* Historia ya miaka elfu mbili sasa imedhihirisha ukweli wa maneno hayo.

***103 - Papa amejaliwa na Mungu mamlaka gani?***

- Papa amejaliwa na Mungu mamlaka kamili juu ya waamini wote awafungulie ufalme wa mbinguni, kama Yesu alivyomuambia Petro: "Nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni; na lolote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni, na lolote utakalolifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni" *(Math 16:19).* "Nimekuombea wewe ili imani yako isitindike; nawe utakapoongoka waimarishe ndugu zako" *(Lk 22:32).* "Lisha wanakondoo wangu… Chunga kondoo zangu…

Lisha kondoo zangu" *(Yoh 21:15-17).*

***104 - Maaskofu wote wamerithi mamlaka gani?***

- Maaskofu wote wamerithi mamlaka ya Mitume kwa kufundisha, kutakasa na kuongoza Kanisa lote pamoja na Papa na chini yake. Wale waliokabidhiwa jimbo fulani ni msingi wa umoja kwa waamini wao na kati yao na Kanisa lote duniani. "Jitunzeni nafsi zenu, na lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa lake Mungu, alilolinunua kwa damu yake mwenyewe" *(Mdo 20:28).*

***105 - Maaskofu wanasaidiwa na nani?***

- Maaskofu wanasaidiwa kwanza na mapadri katika uchungaji, halafu na mashemasi katika utumishi. "Nawasihi wazee walio kwenu, mimi niliye mzee, mwenzi wao, na shahidi wa mateso ya Kristo, na mshirika wa utukufu utakaofunuliwa baadaye: lichungeni kundi la Mungu lililo kwenu, na kulisimamia" *(1Pet 5:1-2).* "Paulo na Timotheo, watumwa wa Kristo Yesu, kwa watakatifu wote katika Kristo Yesu, walioko Filipi, pamoja na Maaskofu na mashemasi" *(Fil 1:1).*

***106 - Bila ya Maaskofu, mapadri na mashemasi, Kanisa lingekuwaje?***

- Bila ya Maaskofu, mapadri na mashemasi, Kanisa lisingekuwepo kwa sababu uhai wake unategemea kabisa ekaristi iliyokabidhiwa kwao. "Mkate ule tuumegao, si ushirika wa mwili wa Kristo? Kwa kuwa mkate ni mmoja, sisi tulio wengi tu mwili mmoja; kwa maana sisi sote twapokea sehemu ya ule mkate mmoja" *(1Kor 10:16-17).* Bila ya ekaristi tusingekuwa Kanisa, bali jumuia tu, kama madhehebu mengi yaliyojichagulia viongozi wasioshirikishwa hizo daraja takatifu kwa kuwekewa mikono na mwandamizi wa Mitume. "Uichochee karama ya Mungu, iliyo ndani yako kwa kuwekewa mikono yangu" *(2Tim 1:6).* "Nalikuacha Krete, ili uyatengeneze yaliyopunguka, na kuweka wazee katika kila mji kama vile nilivyokuamuru" *(Tit 1:5).* "Usimwekee mtu

mikono kwa haraka" *(1Tim 5:22).*

***107 - Walei wanaitwa na Mungu kufanya nini?***

- Walei wanaitwa na Mungu kuratibu malimwengu yote yafuate matakwa yake. "Wapeni wote haki zao; mtu wa kodi, kodi; mtu wa ushuru, ushuru; astahiliye hofu, hofu; astahiliye heshima, heshima" *(Rom 13:7).* "Uwakumbushe watu kunyenyekea kwa wenye uwezo na mamlaka, na kutii, na kuwa tayari kwa kila kazi njema" *(Tit 3:1).* "Kwa sababu ndiyo mapenzi ya Mungu, kwamba kwa kutenda mema mzibe vinywa vya ujinga vya watu wapumbavu; kama walio huru, ila wasioutumia uhuru huo kwa kusitiri ubaya, bali kama watumwa wa Mungu" *(1Pet 2:15-16).*

***108 - Watawa wanashika mashauri gani ya Kiinjili?***

- Watawa wanashika hasa mashauri ya useja mtakatifu, ufukara na utiifu ambayo msingi wake ni maisha na mafundisho ya Yesu kadiri ya Injili. "Wako matowashi waliojifanya kuwa matowashi kwa ajili ya ufalme wa mbinguni. Awezaye kulipokea neno hili, na alipokee" *(Math 19:12).* "Ukitaka kuwa mkamilifu, enenda ukauze ulivyo navyo, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni; kisha njoo unifuate" *(Math 19:21).* "Ninyi mmekuwa rafiki zangu, mkitenda niwaamuruyo" *(Yoh 15:14).*

***109 - Ushirika wa watakatifu maana yake nini?***

- Ushirika wa watakatifu maana yake sisi, kwa kushiriki mafumbo matakatifu tunaunda ndani ya Kristo mwili mmoja, ambamo waadilifu waliopo duniani, marehemu wa toharani na wenye heri wa mbinguni tunaunganishwa na upendo tufaidike na mema ya kila mmoja. "Kwa maana kama tukiishi, twaishi kwa Bwana, au kama tukifa, twafa kwa Bwana. Basi kama tukiishi au kama tukifa, tu mali ya Bwana. Maana Kristo alikufa akawa hai tena kwa sababu hii, awamiliki waliokufa na walio hai pia" *(Rom 14:8-9).* "Kiungo kimoja kikiumia, viungo vyote huumia nacho, na kiungo kimoja kikitukuzwa, viungo vyote hufurahi

pamoja nacho. Basi ninyi mmekuwa mwili wa Kristo, na viungo kila kimoja peke yake" *(1Kor 12:26-27).* Dhambi yoyote kubwa inatutenga na ushirika huo kama Yesu alivyosema, "Mimi ndimi mzabibu wa kweli, na Baba yangu ndiye mkulima. Kila tawi ndani yangu lisilozaa huliondoa" *(Yoh 15:1-2).* Lakini "Mungu aweza kuwapandikiza tena... Kwa sababu karama za Mungu hazina majuto, wala mwito wake" *(Rom 11:23,29).*

***110 - Je, Kanisa linaweza kutuondolea dhambi yoyote?***

- Ndiyo, Kanisa linaweza kutuondolea dhambi yoyote katika ubatizo na kitubio kwa kutumia mamlaka ambayo Yesu mfufuka aliwashirikisha Mitume wake alipowavuvia akisema: "Pokeeni Roho Mtakatifu. Wowote mtakaowaondolea dhambi, wameondolewa; na wowote mtakaowafungia dhambi, wamefungiwa" *(Yoh 20:22-23).* "Mlikuwa watu wa namna hii; lakini mlioshwa, lakini mlitakaswa, lakini mlihesabiwa haki katika jina la Bwana Yesu Kristo, na katika Roho wa Mungu wetu" *(1Kor 6:11).*

***111 - Je, ni muhimu tujiandae kufa?***

- Ndiyo, ni muhimu tujiandae kufa wakati wowote na namna yoyote kwa kuishi kitakatifu sasa na kwa kujiombea neema tutakazohitaji saa ya kufa kwetu, tukijua tumewekewa "kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu" *(Eb 9:27).* "Katika mambo yako yote uukumbuke mwisho wako, hivyo hutakosa kamwe hata hatima" *(YbS 7:36).* "Hamjui yatakayokuwako kesho! Uzima wenu ni nini? Maana ninyi ni mvuke uonekanao kwa kitambo, kisha hutoweka" *(Yak 4:14).* "Kesheni, mwombe, msije mkaingia majaribuni" *(Math 26:41).*

***112 - Je, ina thamani machoni pa Bwana mauti ya mtu aliyemcha?***

- Ndiyo, "ina thamani machoni pa Bwana mauti ya wacha Mungu wake" *(Zab 116:15).* Hasa utiifu wa Yesu msalabani umegeuza laana ya kifo iwe baraka kwa waamini wake. "Heri wafu wafao katika Bwana tangu sasa. Naam, asema Roho, wapate kupumzika baada ya taabu zao; kwa kuwa matendo yao yafuatana nao" *(Ufu 14:13).*

***113 - Tutakapofariki dunia itatutokea nini?***

- Tutakapofariki dunia roho yetu isiyokufa, mbali na mwili unaooza, itapewa tuzo au adhabu tuliyostahili kwa maisha yetu. "Ikawa yule maskini alikufa, akachukuliwa na malaika mpaka kifuani kwa Ibrahimu. Yule tajiri naye akafa, akazikwa. Basi, kule kuzimu aliyainua macho yake, alipokuwa katika mateso, akamwona Ibrahimu kwa mbali, na Lazaro kifuani mwake" *(Lk 16:22-23).* "Kwangu mimi kuishi ni Kristo, na kufa ni faida… ninatamani kwenda zangu nikae na Kristo, maana ni vizuri zaidi sana" *(Fil 1:21,23).* "Nasi tunaona ni afadhali kutokuwamo katika mwili na kukaa pamoja na Bwana" *(2Kor 5:8).* Kwa kuwa kifo ni "mavumbi kuirudia nchi kama yalivyokuwa, nayo roho kumrudia Mungu aliyeitoa" *(Mhu 12:7).* Siku ya ufufuo roho na mwili vitaungana tena kwa ajili ya uzima au moto wa milele. "Pumzi iliwaingia, wakaishi, wakasimama kwa miguu yao, jeshi kubwa mno" *(Ez 37:10).*

***114 - Je, sisi wanyonge tunaweza kushiriki uzima wa milele wa Mungu?***

- Ndiyo, sisi wanyonge tunaweza kushiriki uzima wa milele wa Mungu: hapa duniani katika mwanga hafifu wa imani, na kisha kufa katika uangavu wa utukufu usiofifia kamwe. Kwa kuwa lengo la Baba ni kwamba tuungane na Yesu Mwanae kwa uwezo wa Roho Mtakatifu ili tuwe na utukufu wake. "Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma" *(Yoh 17:3).* "Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe. Tena kwa hayo ametukirimia ahadi kubwa mno, za thamani, ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika wa tabia ya Uungu, mkiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa" *(2Pet 1:3-4).* Sisi tuliobatizwa tunaitwa "wana wa Mungu; na ndivyo tulivyo!" *(1Yoh. 3:1).* Kwa sababu tumesadiki kwamba "Mungu ni upendo" *(1Yoh*

*4:8)* na kwamba "hakuna lisilowezekana kwa Bwana" *(Lk 1:37).* "Na kwa kuwa ninyi mmekuwa wana, Mungu alimtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu, aliaye, 'Aba!' yaani, 'Baba!' Kama ni hivyo, wewe si mtumwa tena bali u mwana; na kama u mwana, basi, u mrithi kwa Mungu" *(Gal 4:6-7).*

***115 - Aliyezungumzia moto wa milele ni nani?***

- Aliyezungumzia moto wa milele ni hasa Yesu: akitufunulia ukuu wa upendo wa Mungu, aliye heri yetu pekee, alituangalisha juu ya hatari ya kutengana naye milele kwa dhambi. Mwenyewe atatoa hukumu hiyo: "Ondokeni kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake" *(Math 25:41).* "Humo funza wao hafi, wala moto hauzimiki" *(Mk 9:48).* "Na moshi wa maumivu yao hupanda juu hata milele na milele, wala hawana raha mchana wala usiku" *(Ufu 14:11).*

***116 - Toharani maana yake nini?***

- Toharani maana yake kuna hali ya muda ambayo huruma ya Mungu inawatakasa marehemu waliofariki dunia katika urafiki naye lakini bila ya usafi kamili unaotakiwa kwa kuingia mbinguni. Sisi tunaweza kuharakisha utakaso wao kwa kumtolea Mungu sala na sadaka, hasa ekaristi. Yuda Mmakabayo "alichanga fedha kwa kila mtu jumla drakma elfu mbili, akazipeleka Yerusalemu kutoa sadaka ya dhambi. Kwa kufanya hivi alitenda vema na kwa haki, kwa kuwa aliukumbuka ufufuo wa wafu. Maana kama asingalitumaini ya kuwa wale waliokufa watafufuka, ingalikuwa kazi bure isiyo na maana kuwaombea wafu. Lakini kwa kuwa aliufikiri utukufu wa thawabu waliowekewa wale wafao katika utauwa, wazo lake lilikuwa takatifu na la kicho. Ndiyo sababu alifanya upatanisho kwa wafu ili wafunguliwe dhambi zao" *(2Mak 12:43-46).* Imani hiyohiyo iliongoza Wakristo wa kwanza kuwafanyia marehemu ibada ambayo haieleweki vizuri, lakini hailaumiwi na Mtume Paulo: "Kama wafu hawafufuliwi kamwe, kwa nini kubatizwa kwa ajili yao?" *(1Kor 15:29).*

***117 - Je, mwili utakaofufuliwa ni huuhuu tulionao sasa?***

- Ndiyo, mwili utakaofufuliwa ni huuhuu tulionao sasa, lakini katika hali tofauti: "hupandwa katika uharibifu; hufufuliwa katika kutokuharibika" *(1Kor 15:42).* Siku ya ufufuo "ndipo watakapomwona Mwana wa Adamu akija katika wingu pamoja na nguvu na utukufu mwingi" *(Lk 21:27).* "Saa yaja ambayo watu wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake. Nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuko wa uzima, na waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu" *(Yoh 5:28-29).* "Na hao watakwenda zao kuingia katika adhabu ya milele; bali wenye haki watakwenda katika uzima wa milele" *(Math 25:46).*

***118 - Siku ya ufufuo Kristo mfalme atatuhukumu vipi?***

- Siku ya ufufuo Kristo mfalme atatuhukumu kwa kudhihirisha misimamo ya watu wote ambao, kwa kupokea au kukataa upendo wa Mungu moyoni mwao, wametenda mema au la. "Imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliyotenda kwa mwili, kadiri alivyopenda, kwamba ni mema au mabaya" *(2Kor 5:10).* "Basi ninyi msihukumu neno kabla ya wakati wake, hata ajapo Bwana; ambaye atayamulikisha yaliyositirika ya giza, na kuyadhihirisha mashauri ya mioyo; ndipo kila mtu atakapoipata sifa yake kwa Mungu" *(1Kor 4:5).* "Hapo atakapokuja Mwana wa Adamu katika utukufu wake, na malaika watakatifu wote pamoja naye, ndipo atakapoketi katika kiti cha utukufu wake. Na mataifa yote watakusanyika mbele zake; naye atawabagua kama vile mchungaji abaguavyo kondoo na mbuzi; atawaweka kondoo mkono wake wa kuume, na mbuzi mkono wake wa kushoto. Kisha Mfalme atawaambia wale walioko mkono wake wa kuume, 'Njoni, mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu; kwa maana nalikuwa na njaa, mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, mkaninywesha; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha; nalikuwa uchi, mkanivika; nalikuwa mgonjwa, mkaja kunitazama; nalikuwa kifungoni,

mkanijia… Amin, nawaambia, kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi'" *(Math 25:31-36,40).* "Heri wenye rehema, maana hao watapata rehema" *(Math 5:7).*

***119 - Baada ya hukumu ya mwisho itakuwaje?***

- Baada ya hukumu ya mwisho, waadilifu watatukuzwa mwili na roho pamoja na Yesu, na ulimwengu pia utageuzwa. "Kama ilivyo ahadi yake, tunatazamia mbingu mpya na nchi mpya, ambayo haki yakaa ndani yake" *(2Pet 3:13).* "Na Roho na Bibi arusi wasema, 'Njoo!' naye asikiaye na aseme, 'Njoo!'… Yeye mwenye kuyashuhudia haya asema, 'Naam, naja upesi'. Amina. Na uje, Bwana Yesu! Neema ya Bwana Yesu na iwe pamoja nanyi nyote. Amina" *(Ufu 22:17,20-21).*

# MUHTASARI: KANUNI YA IMANI

Ndugu, tukariri maneno ya imani ambayo tunaupokea uzima wa Mungu.
Maneno yenyewe ni machache, ila mafumbo yaliyomo ni mazito.
Tuyatunze kwa moyo mnyofu mpaka imani ya sasa
itakapogeuka heri ya kumtazama milele jinsi alivyo.

Section Break (Continuous)

Section Break (Continuous)

## KANUNI YA IMANI YA MITUME

Nasadiki kwa Mungu,
Baba Mwenyezi,
Mwumba mbingu na dunia,

na kwa Yesu Kristo,
Mwanae wa pekee, Bwana wetu,

## KANUNI YA IMANI YA NISEA-KOSTANTINOPOLI

Nasadiki kwa Mungu mmoja,
Baba Mwenyezi,
Mwumba mbingu na nchi,
na vitu vyote vinavyoonekana,
na visivyoonekana.

Nasadiki kwa Bwana mmoja
Yesu Kristo,
Mwana wa pekee wa Mungu.
Aliyezaliwa kwa Baba tangu
milele yote.
Mungu aliyetoka kwa Mungu,

mwanga kwa mwanga,
Mungu kweli kwa Mungu kweli.
Aliyezaliwa bila kuumbwa,
mwenye Umungu mmoja na
Baba;
ambaye vitu vyote vimeumbwa
naye.

End of Section

aliyetungwa
kwa Roho Mtakatifu,
akazaliwa na Bikira Maria,

akateswa kwa mamlaka ya
Ponsio Pilato,
akasulibiwa, akafa, akazikwa;
akashukia kuzimu;
siku ya tatu akafufuka
katika wafu;
akapaa mbinguni,
amekaa kuume kwa Mungu Baba
Mwenyezi;
toka huko atakuja
kuwahukumu wazima na wafu.

Nasadiki kwa Roho Mtakatifu,

Kanisa takatifu
katoliki,

ushirika wa watakatifu,
maondoleo ya dhambi,
ufufuko wa miili,
uzima wa milele.
Amina.
Ameshuka toka mbinguni kwa ajili yetu sisi wanadamu
na kwa ajili ya wokovu wetu.
Akapata mwili
kwa uwezo wa Roho Mtakatifu
kwake yeye Bikira Maria;
akawa mwanadamu.
Akasulibiwa pia kwa ajili yetu sisi;
akateswa kwa mamlaka ya Ponsio Pilato,
akafa, akazikwa.

Akafufuka siku ya tatu,
ilivyoandikwa.
Akapaa mbinguni;
amekaa kuume kwa Baba.
Atakuja tena kwa utukufu
kuwahukumu wazima na wafu;
nao ufalme wake hautakuwa na mwisho.

Nasadiki kwa Roho Mtakatifu,
Bwana mleta uzima;
atokaye kwa Baba na Mwana.
Anayeabudiwa na kutukuzwa
pamoja na Baba na Mwana:
aliyenena kwa vinywa vya Manabii.
Nasadiki Kanisa moja, takatifu, katoliki,
la Mitume.
Naungama ubatizo mmoja
kwa maondoleo ya dhambi.
Nangojea na ufufuko wa wafu.
Na uzima wa milele ijayo.
Amina.

Section Break (Continuous)

Section Break (Continuous)

**Ninasadiki na kuungama yote ambayo Kanisa Takatifu Katoliki linasadiki, linafundisha na kutangaza kwamba hayo yamefumbuliwa na Mungu.**